

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



BUNGE LA TANZANIA

**MAONI NA USHAURI KWA NIABA YA WAJUMBE WA KAMATI YA
BAJETI KUHUSU AZIMIO LA BUNGE LA KURIDHIA MKATABA WA
TAKWIMU WA AFRIKA (*THE AFRICAN CHARTER ON STATISTICS*)
KWA MUJIBU WA MATAKWA YA IBARA 63(3)(3) YA KATIBA YA
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA YA MWAKA 1977.**

Ofisi ya Bunge,
S. L. P 941,
DODOMA

Novemba 2018.

1.0 UTANGULIZI

1.1 Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha maoni na ushauri kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Bajeti kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Takwimu wa Afrika (*The African Charter on Statistics*) kwa mujibu wa matakwa ya Ibara 63(3)(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

1.2 Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba mwaka 2009 Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika waliazimia kuwa na Mkataba wa Takwimu wa Afrika (*The African Charter on Statistics*) kwa lengo la kuweka Mfumo wa kuratibu upatikanaji na usambazaji wa takwimu bora za uchumi, jamii na mazingira zitakazotumika katika kupanga na kutolea maamuzi mbalimbali ya kisera katika ngazi ya Taifa, Kanda na Bara zima la Afrika.

1.3 Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi mojawapo kati ya nchi 32 zilizosaini mkataba huo tarehe 23 Machi 2012; na mpaka sasa nchi 22 zimeridhia Mkataba huo (sawa na asilimia 69) na umeanza kutumika rasmi tarehe 08 Februari, 2015. Hivyo hatua ya kuridhia mkataba huu ni kupata nguvu ya kisheria kwa ajili ya kutekeleza malengo ya Azimio kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

1.4 Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na kuunga mkono Azimio hili ambalo kimsingi litasaidia kuweka mfumo wa pamoja wa kuratibu na kusimamia uzalishaji na usambazaji wa takwimu rasmi kwa ajili ya watumiaji wa ndani na nje ya Bara la Afrika. Nchi zote duniani zinazopiga hatua za maendeleo ya kiuchumi na kijamii zinategemea upatikanaji wa takwimu sahihi ambazo uchakataji wake unasaidia watunga sera na wataalamu wa mipango kushauri ipasavyo kuhusu maendeleo ya nchi kiuchumi na kijamii.

2.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI KUHUSU AZIMIO LA BUNGE LA KURIDHIA MKATABA WA TAKWIMU WA AFRIKA (*THE CHARTER ON STATISTICS*).

Mheshimiwa spika, Kamati imepitia na kujadili vipengele 17 vya Azimio hili ambayo vimeweka misingi Sita ya Azimio hili yaani; uhuru wa kitaaluma, ubora wa takwimu, mamlaka ya kutoa takwimu na upatikanaji wa rasimali, usambazaji wa takwimu, kulinda na kutoa taarifa za takwimu, uratibu na ushirikiano baina ya wadau wa takwimu pamoja na utekelezaji wa Makataba katika Nchi Wanachama. Kwa mantiki hii Kamati inapenda kutoa maoni na ushauri ufuatao:-

2.1 Mheshimiwa Spika, kamati inaipongeza Serikali kwa kuleta Azimio hili ambalo kimsingi litasaidia kuwa na ulinganifu wa takwimu ulio bora baina ya nchi za Afrika katika viashiria vya kiuchumi na kijamii. Hatua hii itasaidia kuongeza ushindani wa maendeleo katika sekta mbalimbali kama vile kilimo, madini, uzalishaji viwandani, ujenzi, utoaji wa huduma, usafirishaji, mawasiliano na huduma za fedha

na hivyo kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Mwaka 2025 na malengo endelevu ya Maendeleo ya Dunia ya Mwaka 2030 na Agenda ya Afrika ya Mwaka 2063.

2.2 Mheshimiwa Spika, Tanzania inatambua umuhimu wa takwimu kwa maendeleo ya uchumi na jamii hatua iliyosababisha kutungwa kwa Sheria ya Takwimu ya Mwaka 2015 (The Statistics Act. Cap 351) na kufanyiwa marekebisho mwaka 2018. Kamati inapenda kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa maudhui mazuri yaliyopo katika Mkataba huu kwa kiwango kikubwa yamejumuishwa katika Sheria ya Takwimu iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2018. Kwa mfano Sheria ya Sasa kupitia kifungu cha Nne (4) cha Sheria hiyo, imeanzisha na kuipa Ofisi ya Taifa ya Takwimu mamlaka kamili (*autonomous*) ya kutekeleza majukumu yake kama inavyoelekezwa kwenye Mkataba unaopendekezwa kuridhiwa.

Mheshimiwa Spika, aidha Sheria hiyo imeweka misingi ya kulinda na kuendeleza uadilifu (*integrity*) na kutofungamana (*impartiality*) na mtu yoyote au taasisi yenye maslahi na

takwimu husika. Vilevile Sheria hii imeweka utaratibu wa ukusanyaji, uchakataji, utoaji na usambazaji wa takwimu.

2.3 Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Azimio hili imeeleza kwa kina malengo ya Mkataba unaoridhiwa ambayo kimsingi yatasaidia nchi kupiga hatua katika kuzalisha, kusimamia na kusambaza taarifa za takwimu katika ngazi mbalimbali za Kitaifa na Kimataifa. Hatua hii itasaidia kuwa na matumizi na uimarishaji bora wa takwimu zinazotakiwa katika kusimamia uchumi na jamii ndani ya nchi pamoja na ushirikiano wa kikanda barani Afrika.

2.4 Mheshimiwa Spika, kuridhiwa kwa azimio la Mkataba huu wa Takwimu kutasaidia kujenga maadili ya watakwimu pamoja na kuboresha uratibu wa shughuli za takwimu na taasisi za takwimu. Hata hivyo, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kunakuwepo na uwazi, ubora na usahihi wa utelewaji wa taarifa za kitakwimu pamoja na matumizi yake kutoka kwa wadau ambao watapaswa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za nchi.

2.5 Mheshimiwa Spika, kupitia Azimio hili, Watakwimu watakuwa na uhuru wa kitaaluma wa kutekeleza majukumu yao bila ya kuingiliwa na mamlaka ya kisiasa au kundi lolote lenye maslahi na Takwimu. Pamoja na hatua hii nzuri ya uhuru wa Watakwimu, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kuwa shughuli za Watakwimu zinazingatia sheria, taratibu na kanuni za nchi ili misingi ya Mkataba huu itekelezwe bila kuwepo na mgongano wa kimaslahi kwa watoaji na watumiaji wa takwimu ndani na nje ya nchi.

2.6 Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali kuwa kupitia Azimio hili ianze kuweka mikakati mbalimbali ya kuondoa au kupunguza changamoto mbalimbali zilizopo katika uzalishaji wa takwimu kama vile uhaba wa rasilimali kwa ajili ya uzalishaji wa takwimu, ukosefu wa uhakika wa teknolojia za kisasa, kutofanyika kwa tafiti kwa mujibu wa kalenda za utafiti, pamoja na upungufu wa matumizi ya takwimu za kiutawala. Hatua hii itasaidia kuimarisha na kuratibu uzalishaji na utolewaji wa takwimu bora zitakazotumika katika kupanga na kutolea maamuzi mbalimbali ya kisera pamoja na mipango ya maendeleo.

2.7 Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kuwa kuridhiwa kwa Mkataba huu wa Takwimu, Tanzania kama Nchi mwanachama itawajibika kuhakikisha Mamlaka za takwimu zinakuwa na rasilimali za kutosha na za kuaminika ili kuwezesha kutimiza matakwa ya takwimu kitaifa, kikanda na kwa Bara la Afrika. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuanza kufikiria kutenga rasilimali watu, nyenzo na fedha za kutosha ambazo zitatakiwa kutumika kwa uangalifu na hivyo kutimiza malengo yaliyokusudiwa.

2.8 Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kuwa Mamlaka za Takwimu, watakwimu na wote wanaojishughulisha na tasnia ya takwimu wanapaswa kuhakikisha uwepo wa ulinzi wa maisha binafsi, siri za kibiashara za watoa taarifa kama vile makampuni, taasisi za umma n.k, usiri wa taarifa zilizotolewa na taarifa hizo zitumike kwa malengo ya takwimu tu. Aidha, taarifa zinazomhusu mtu au taasisi zilizokusanywa kwa ajili ya takwimu kwa namna yoyote ile zisitumike katika mwenendo

wa mahakama, hatua za adhabu au kufanya maamuzi ya kiutawala dhidi ya mtoa taarifa.

2.9 Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa maelezo ya Serikali, Mkataba huu wa Takwimu utahifadhiwa katika lugha ya rasmi ya Kiarabu, Kiingereza, Kireno, na Kifaransa. Kamati inashauri Serikali kusimamia na kuhakikisha kuwa Mkataba huu unahifadhiwa pia katika lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maoni na ushauri uliotolewa na Kamati hapo juu, Kamati inaona kuwa Mkataba huu ukiridhiwa utakuwa na manufaa kwa maendeleo ya Taifa kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni kama ifuatavyo:-

- i) Kutakuwepo na uhakika wa ulinganifu wa takwimu ulio bora zaidi wa viashiria vya kiuchumi na kijamii baina ya nchi za Afrika; Kutokana na kuwepo kwa mfumo imara wa uzalishaji takwimu rasmi zinazokidhi viwango vinavyokubalika katika mfumo wa Takwimu wa Afrika (*Africa Statistical System*);

- ii) Kutaongezeka ubora wa takwimu rasmi za Serikali na hatimaye kuongezeka kwa matumizi ya takwimu hizo kitaifa na kimataifa. Hali hiyo itachochea uwekezaji wa ndani na nje ya nchi na hivyo kuchangia kwa kiasi kikubwa ukuaji wa uchumi, kupunguza umaskini, kuongezeka kwa mapato ya Serikali na ajira;
- iii) Watakwimu nchini watajengewa uwezo zaidi wa mbinu za kisasa za matumizi ya teknolojia kwa ajili ya kuboresha uzalishaji wa takwimu rasmi zitakazohitajika katika kufuatilia na kutathimini viashiria vya kiuchumi na kijamii kwa kutumia ushirikiano uliopo mionganoni mwa nchi wanachama;
- iv) Nchi itaendelea kufaidika na misaada ya kibajeti na kitaalam katika kuboresha na kuimarisha tasnia ya takwimu itakayotolewa katika Bara la Afrika na wadau wa mbalimbali wakiwemo wa maendeleo, sekta binafsi na wengine; na

v) Nchi itakuwa na fursa ya kupata misaada ya kibajeti na kitaalamu katika kuboresha na kuimarisha mifumo ya takwimu katika ngazi mbalimbali za utawala Nchini.

3.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kwanza kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika kwa miongozo yako na kunipa fursa kuwasilisha Taarifa hii ya Kamati. Aidha, nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Naibu Spika kwa miongozo yake. Vilevile, napenda nimshukuru Dkt. Philip Mpango (Mb), Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji (Mb), Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao walioutoa kwa Kamati. Pia napenda kumshukuru Dkt. Albina Chuwa, Mkurugenzi Mkuu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushirikiano walioutoa katika kipindi chote cha kuchambua na kupitia Azimio hili.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi, Makamu

Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Wajumbe wote wa Kamati hii kwa umahiri wao katika kupitia na kujadili Azimio hili na kuweza kuboresha hadi kufikia hatua hii. Naomba niwatambue Wajumbe hao kama ifuatavyo;

1. Mhe. George Boniface Simbachawene, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb – Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. David Ernest Silinde, Mb
4. Mhe. Dkt. Immaculate Sware Semesi, Mb
5. Mhe. Mbaraka Kitwana Dau, Mb
6. Mhe. Mendrad Lutengano Kigola, Mb
7. Mhe. Maria Ndilla Kangoye, Mb
8. Mhe. Oran Manase Njeza, Mb
9. Mhe. Riziki Said Lulida, Mb
10. Mhe. Freeman Aikael Mbowe, Mb
11. Mhe. Hasna Sudi Katunda Mwilima, Mb
12. Mhe. Makame Kassim Makame, Mb
13. Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajab, Mb
14. Mhe. Abdallah Majura Bulembo, Mb
15. Mhe. Prof. Anna Kajumulo Tibaijuka, Mb
16. Mhe. Ibrahim Hassanali Mohammedali Raza, Mb

- 17.Mhe. Stephen Julius Masele, Mb
- 18.Mhe. Ali Hassan Omari, Mb
- 19.Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb
- 20.Mhe. Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mb
21. Mhe. Albert Obama Ntabaliba, Mb
- 22.Mhe. Andrew John Chenge, Mb
- 23.Mhe. Suleiman A. Sadiq, Mb
- 24.Mhe. Shally J. Raymond, Mb
- 25.Mhe. Hussein M. Bashe, Mb

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee kabisa, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Ndg. Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge kwa kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake katika kipindi chote. Aidha, napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Kaimu Mkurugenzi Ndugu Lina Kitosi, Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Michael Kadebe na Makatibu wa Kamati hii Ndugu Godfrey Godwin, Emmanuel Rhobi, Lilian Masabala, Maombi Kakozi kwa kuratibu shughuli za Kamati na kukamilisha taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda pia kuwashukuru Wanasheria wa Ofisi ya Bunge Ndg. Mossy Lukuvi, Matamus

Fungo, Nesta Kawamala, Stephano Mbutu, Thomas Shawa na Maria Mdulugu kwa kutoa ushauri wao wa kisheria uliosaidia kukamilisha kwa taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Kamati imetafakari kwa kina manufaa yatokanayo na Mkataba huu pamoja na umuhimu wake kwa maendeleo ya Taifa na hivyo inashauri Bunge lako tukufu liazmie na kuridhia Mkataba wa Takwimu wa Afrika (*The African Charter on Statistics*) kama ilivyowasilishwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono Azimio hili.



Mhe. George Boniface Simbachawene, Mb.

MWENYEKITI

KAMATI YA BUNGE YA BAJETI

14 Novemba, 2018